WIZARA YA NISHATI

# NewsBulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 71 | Okt 1 - 30 2025



# MAABARA ZA UBORA NA UFANISI WA NISHATI ZAZINDULIWA TBS

WIZARA YA NISHATI    +255-26-2320148 AU +255-26-232018

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**
Dkt. James Mataragio

**MHARIRI**
Neema Chalila Mbuja
Teresia Mhagama

**WAANDISHI**
Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Felista Charles
Petro Mwanda
Judith Hasani

**WAPIGA PICHA**
Henry Kilasila
Godfrey Mwemezi
Ruben Richard
Amanzi Kimonjo

**MSANIFU KURASA**
Brian Mbaga

© NISHATI 2025


NISHATI SAFI YA KUPIKIA
OKOA MAISHA
NA MAZINGIRA
45

# MAABARA TANO ZA KITAIFA ZA KUPIMA UBORA NA UFANISI WA MATUMIZI YA NISHATI NA KIWANGO CHA CHINI CHA UFANISI WA MATUMIZI YA NISHATI ZAZINDULIWA

- Zitapima viwango vya matumizi bora ya Umeme katika Luninga, Viyoyozi, Friji,Feni na Mota za Umeme
- Kupunguza gharama za matumizi ya umeme Majumbani
- Kuongeza ufanisi wa Nishati Safi ya Kupikia



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Dkt. James Mataragio akihutubia wadau mbalimbali waliohudhuria katika uzinduzi wa Maabara Tano za Kitaifa za kupima Ubora na Ufanisi wa Matumizi ya Nishati Jijini Dar es Salaam.

Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya( EU) imezindua maabara tano za Taifa zitakazopima Ubora na Ufanisi wa Matumizi bora ya Nishati pamoja na Kiwango cha Chini cha Ufanisi wa Matumizi ya Nishati pamoja na mfumo wa uwekaji alama za nishati.

Pia kimezinduliwa kifaa cha kupima kiwango cha hewa ya ukaa inayozalishwa katika majiko.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika tarehe 16 Oktoba 2025 jijini Dar es Salaam, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio amesema kuwa maabara hizo zimekuja kwa wakati sahihi kwa kuwa tayari Serikali inatekeleza sera na mikakati mbalimbali ya nishati nchini.

Maabara hizo pamoja na kifaa hicho cha kupima hewa ya ukaa vinapatikana katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Dkt. Mataragio amesema miradi hiyo italeta mabadiliko makubwa nchini katika matumizi bora ya nishati, Matumizi ya nishati safi ya kupikia, kuongeza juhudi za kutunza mazingira na kupunguza gharama za matumizi ya umeme kwa wananchi.

"Ni wakati wa kujivunia kama taifa tunapochukua hatua mahsusi kuhakikisha kila kifaa kinachotumika majumbani, maofisini, na viwandani kinachangia matumizi sahihi na yenye ufanisi wa nishati, na hii ni dhamira ya dhati ya serikali yetu kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa huduma za nishati za kisasa, nafuu, na salama kwa wote huku kukiwa na matumizi bora ya nishati kwa maendeleo ya kiuchumi na kijami." Amesema Dkt. Mataragio

Amesema kuwa maabara na Viwango vilivyozinduliwa vitahakikisha kuwa ni bidhaa zenye ubora na ufanisi pekee ndizo zinazoingia sokoni, hivyo kupunguza matumizi ya umeme, gharama kwa watumiaji, na uzalishaji wa hewa ya ukaa.

Utekelezaji wa mradi huo kwa pamoja vinachangia zaidi ya asilimia 45 ya matumizi ya umeme nchini kitaifa huku uwekaji wa viwango vya ufanisi unatarajia kuokoa zaidi ya 370 GWh za umeme kila mwaka kufikia 2030, sawa na kuupatia umeme zaidi ya nyumba 500,000 kila mwaka na kupunguza zaidi ya tani 250,000 za hewa ya ukaa ($CO_2$) kila mwaka.

Viwango vya friji na viyoyozi vimeidhinishwa katika ngazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), jambo linalowanufaisha watumiaji na wazalishaji wa Tanzania kupitia soko la kikanda lenye ubora, usalama, na uendelevu.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dkt. Ashura Katunzi amesema kuwa baada ya uzinduzi huo kinachofuata sasa na utoaji wa elimu sahihi juu kwa wadau mbalimbali ikiwamo wazalishaji wa bidhaa tajwa ili waweze kuanza kutumia maabara hizo.

Aidha elimu itatolewa kwa wananchi kununua na kutumia bidhaa zenye nembo ya ubora iliyozinduliwa nchini.

Naye Mkuu wa Ushirikiano kutoka EU, Mark Stalmans amesema utekelezaji wa miradi hiyo ni matokeo mazuri ya ushirikiano baina Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Ulaya katika ufanisi wa utekelezaji wa miradi mbalimbali inayoendela kutekelezwa nchini Tanzania.

Amesisitiza kuwa uzinduzi huo utoe matokeo chanya katika usimamizi wa masoko, ufuatiliaji, tathmini pamoja na utekelezaji wa uwekaji mfumo wa alama ili kulinda watumiaji na ubora wa bidhaa.


Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Dr. James Mataragio aliposhiriki Uzinduzi wa Maabara tano za Kitaifa za Kupima Ubora na Ufanisi wa Matumizi ya Nishati na Kiwango cha chini cha ufanisi wa Matumizi ya Nishati.





# MRADI WA TAZA KUFUNGUA SOKO JIPYA LA BIASHARA YA UMEME AFRIKA

- Wafikia asilimia 83
- Dkt. Mataragio akagua mradi na kutoa maelekezo TANESCO
- TAZA kuunganisha Mkoa wa Rukwa na gridi ya Taifa
- Kuimarisha upatikanaji umeme Mikoa ya Kusini mwa Tanzania



Naibu katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio pamoja na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Mha. Innocent Luoga mara baada ya kupokelewa walipoenda kutembelea mradi wa TAZA katika eneo la Iganjo.

Imeelezwa kuwa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Zambia kupitia Tunduma (TAZA) umefikia asilimia 83.45 huku ukitarajiwa kukamilika ifikapo Mei 2026 na hivyo kufungua soko jipya la biashara ya umeme barani Afrika.

Akizungumza wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi huo katika eneo la Iganjo, Mbeya, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio amesema mradi wa TAZA ni muhimu kwa Taifa kwa kuwa utaiunganisha Tanzania na Nchi za ukanda wa Kusini mwa Afrika (Southern Africa Power Pool) na pia kuimarisha muunganiko wa ukanda wa Mashariki mwa Afrika (East Africa Power Pool).

"Nimshukuru na kumpongeza Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya nishati. Kupitia mradi huu tutaimarisha biashara ya kuuza na kununua umeme kati ya nchi za Mashariki mwa Afrika na zile zilizopo Kusini mwa Afrika". Amesema Dkt. Mataragio

Kuhusu biashara ya umeme ya kikanda, Dkt. Mataragio amesema kuwa tayari Tanzania imeshaunganisha gridi ya umeme na Nchi za Afrika za Kenya, Rwanda, Burundi na Ethiopia kupitia muunganiko wa East Africa Power Pool.

"Tutaunganisha pia gridi na nchi za Kaskazini na Magharibi mwa Afrika ili Afrika nzima tuweze kuuziana umeme ikiwa ni sehemu pia ya kutekeleza Mpango wa Nishati unaolenga kuwafikishia umeme waafrika takribani milioni 600 ambao bado hawajafikiwa na nishati ya umeme". Amesisitiza Dkt. Mataragio.

Kuhusu mradi wa TAZA, ameeleza kuwa unatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ambao ni Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya na Shirika la Maendeleo la Ufaransa kwa Dola za kimarekani milioni 584.

Amesema kuwa mbali ya mradi wa TAZA kuunganisha gridi za umeme za Nchi za Kusini mwa Afrika, utauunganisha Mkoa wa Rukwa na umeme wa gridi pamoja na kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe.

Baada ya kukagua mradi huo, Dkt. Mataragio ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuhakikisha linamsimamia Mkandarasi kwa karibu hasa katika kipindi hiki cha mvua ili hatua za awali za ujenzi wa misingi (foundation) ziweze kukamilika kwa wakati na kumtaka Mkandarasi kuhakikisha vifaa vyote vipo eneo la Mradi.

Katika hatua nyingine Dkt. Mataragio ameiagiza TANESCO kuhakikisha inapeleka umeme eneo la Ngozi unapotekelezwa mradi wa kuzalisha umeme kwa jotoardhi ambapo kwa hivi sasa mitambo ya uhakiki wa jotoardhi katika eneo hilo inatumia mafuta ya dizeli.

Katika ziara hiyo Naibu Katibu Mkuu aliambatana na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Mha. Innocent Luoga na watendaji wa Wizara ya Nishati na TANESCO.



Naibu katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio akikaguwa mradi wa TAZA katika eneo la Iganjo Jijini Mbeya, na kutazama shughuli za ujenzi wa mradi huo zinavyo endelea.

# NISHATI YAWASILISHA MIPANGO YA KIMKAKATI KUTEKELEZA DIRA YA TAIFA 2050

- Ni katika kikao kazi na Tume ya Taifa ya Mipango.
- Mradi wa usafirishaji umeme Chalinze–Dodoma ni miongoni mwa miradi ya kipaumbele kufanikisha Dira 2050
- Wizara ya Nishati na Tume ya Mipango kushirikiana kwa karibu kusimamia miradi ya Nishati kufanikisha malengo ya Dira 2050

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, amekutana na wataalam kutoka Tume ya Taifa ya Mipango wakiongozwa na Naibu Katibu Mtendaji – Menejimenti ya Utendaji na Tathmini, Dkt. Linda Ezekiel kwa lengo la kujadili namna ambavyo Wizara na Taasisi zake zimejipanga kutekeleza miradi ya kimkakati ya nishati inayochangia katika kufanikisha malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Msingi wa kikao hicho umetokana na Sekta ya Nishati kuainishwa katika Dira 2050 kuwa ni moja ya vichocheo vitano vitakavyoongeza kasi ya kufikia malengo ya Dira hiyo, ikielezwa kuwa Nishati ya uhakika ni nyenzo muhimu katika kuchochea maendeleo ya viwanda na shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuboresha viwango



Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, (wakwanza kulia) akiwa na wataalam kutoka Tume ya Taifa ya Mipango wakiongozwa na Naibu Katibu Mtendaji Menejimenti ya Utendaji na Tathmini, Dkt. Linda Ezekiel.

vya maisha kwa kutoa fursa za ajira kwa maendeleo endelevu katika jamii.

Katika kikao hicho kilichofanyika jijini Dodoma na kuhusisha Watendaji kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati,

Mha. Mramba amesema pande hizo mbili zimejipanga kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa miradi



Picha ya Pamoja wataalam kutoka Tume ya Taifa ya Mipango wakiongozwa na Naibu Katibu Mtendaji Menejimenti ya Utendaji na Tathmini, Dkt. Linda Ezekiel

ya nishati ili kuhakikisha kuwa inalingana na vipaumbele vya kitaifa vya maendeleo.

"Wizara ya Nishati inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya nishati ukiwemo mradi wa kusafirisha umeme wa kV 400 wa Chalinze–Dodoma, ambao unatarajiwa kukamilika Juni 2026. Huu ni moja ya miradi itakayoleta chachu ya kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika mikoa ya Katavi, Kigoma na maeneo mengine ambayo yamekuwa yakikabiliwa na changamoto za upatikanaji wa umeme thabiti." Amesema Mhandisi Mramba

Amesema kukamilika kwa miradi ya kimkakati ya umeme kutawezesha kutimiza moja ya shabaha katika Dira 2050 ambayo inaelekeza kuwa matumizi ya umeme yanapaswa kuongezeka na kufikia wastani wa Kwh 3,000 kwa kila mtu kwa mwaka.

"Tunataka kuwa Taifa lenye nishati ya uhakika, nafuu na safi kwa watanzania wote, ili kutimiza lengo hili Serikali inawakaribisha wadau wa sekta binafsi kuwekeza katika miradi ya nishati kwa kuwa mafanikio ya sekta hii yanategemea ushirikiano wa wadau wote. " Amesisitiza Mhandisi Mramba

Katika kikao hicho, Wizara pia iliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya Gesi Asilia na Mafuta, Nishati Safi ya Kupikia, Umeme na Nishati Mbadala.

Kwa upande wake, Dkt. Linda Ezekiel kutoka Tume ya Taifa ya Mipango, amepongeza ushirikiano uliopo kati ya Wizara ya Nishati na Tume hiyo akisisitiza kuwa mwelekeo wa miradi iliyoainishwa katika kikao hicho inaendana na malengo ya Dira 2050.

Amesema Tume itaendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo ili kuhakikisha inachangia moja kwa moja katika ukuaji wa uchumi wa Taifa, kuboresha ustawi wa wananchi, na kulinda mazingira.

"DIRA ya 2050 inalenga kuwa na Taifa lenye uchumi wa kisasa, shindani na jumuishi. Sekta ya Nishati ni mhimili wa kufanikisha hayo yote, tunapongeza jitihada za Wizara ya Nishati katika kuhakikisha nishati inakuwa injini ya maendeleo." Ameeleza Dkt. Ezekiel

Kupitia kikao hicho, Wizara ya Nishati na Tume ya Taifa ya Mipango zimekubaliana kuendelea kushirikiana kwa karibu katika kupanga, kutekeleza na kufuatilia miradi yote inayogusa Sekta ya Nishati ili kuhakikisha Tanzania inafikia malengo ya DIRA ya Maendeleo 2050 kwa ufanisi.



# SEKONDARI YA MORINGE SOKOINE YAPEWA ELIMU YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

- Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia awaasa wanafunzi kujifunza teknolojia za nishati safi ya kupikia
- Awahamasisha kuwa mabalozi wa nishati safi ya kupikia

Imeelezwa kuwa, familia nyingi nchini bado zinatumia kuni na mkaa kama vyanzo vikuu vya nishati safi ya kupikia, vyanzo ambavyo vina athari kubwa kwa afya, mazingira, na uchumi.

Kutokana na hilo, Serikali kupitia Wizara ya Nishati, imekuwa mstari wa mbele kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kama vile gesi, umeme na matumizi ya majiko banifu pamoja na kuhakikisha kuwa nishati hizo safi zinawafikia wananchi.



Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia kutoka Wizara ya Nishati, Nolasco Mlay wakati aliposhiriki mahafali ya kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Moringe Sokoine iliyopo wilayani Monduli mkoani Arusha akiwa ni mgeni rasmi.

Hayo yamesemwa leo na Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia kutoka Wizara ya Nishati, Nolasco Mlay wakati aliposhiriki mahafali ya kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Moringe Sokoine iliyopo wilayani Monduli mkoani Arusha akiwa ni mgeni rasmi.

Mlay amesema tafiti zinaonesha kuwa moshi wa kuni na mkaa unasababisha magonjwa ya mfumo wa hewa hasa kwa wanawake na watoto, pia ukataji miti kupita kiasi kwa ajili ya mkaa unachangia ukame na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Amesema matumizi ya kuni pia yana athari ikiwemo za kiuchumi na elimu kwani muda mwingi hutumika kutafuta nishati hiyo hivyo kupunguza muda wa kufanya shughuli za kiuchumi na kujisomea kwa wanafunzi.

"Ninawahimiza ninyi wahitimu kuwa mabalozi wa mabadiliko haya ya nishati safi ya kupikia, elimisheni familia zenu kuhusu faida za kupika kwa kutumia nishati safi, sambamba na hilo jifunzeni teknolojia mpya kama vile utengenezaji wa majiko banifu au miradi ya bayogesi kwa wafugaji na uzalishaji wa mkaa mbadala." Amesema Mlay

Kwa upande wao, Wanafunzi wa Moringe Sokoine, Wazazi na Wananchi wamemshukuru Mkurugenzi wa Nishati safi ya kupikia kwa kushiriki mahafali hiyo na kupata elimu ya Nishati safi ya Kupikia.



Wananchi mbalimbali waliohudhuria mafunzo ya Nishati safi ya kupikia katika mahafali ya kidato cha Nne katika shule ya Sekondari ya Moringe Sokoine Wilayani Monduli Jijini Arusha.

# TANZANIA KUZINDUA MAABARA ZA KISASA ZA KUPIMA MATUMIZI BORA YA NISHATI

- Lengo ni kupima na kuthibitisha ubora na ufanisi wa vifaa vya umeme vinavyoingizwa nchini
- Kusaidia kuwepo kwa umeme wa ziada katika Gridi na Kudhibiti Upotevu




Kamishna na Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga akizungumza na Waandishi wa Habari jijini Dar es Salaam

Serikali kwa Kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), kupitia ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) watazindua Viwango Fanisi vya Chini vya Nishati (Minimum Energy Performance Standards – MEPS) na Maabara za Upimaji wa Ufanisi wa Nishati. Uzinduzi huo umefanyika jijini Dar es Salaam katika Makao Makuu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Kamishna na Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga amesema hayo wakati akizungumza na Waandishi wa Habari jijini Dar es Salaam ambapo amesema kuwa lengo la kuanzishwa kwa maabara hiyo ni kuhakikisha kuwa vifaa vinavyotumika nchini vinatumia nishati kwa ufanisi kwa lengo la kupunguza gharama kwa watumiaji na kulinda mazingira dhidi ya uzalishaji wa hewa ukaa.

Ameongeza kuwa juhudi hizo zitasaidia kupatikana kwa umeme wa ziada kwenye gridi ya taifa na kutumika katika maeneo mengine ya nchi yenye upungufu wa umeme na kuweza kuwafikia wateja wengine wapya.

Amesema kupitia mradi huo, Tanzania itazindua viwango vya kwanza vya chini vya matumizi ya nishati ya umeme vinavojulikana kama MEPS kwa vifaa vitano vya kipaumbele ambavyo vinachangia matumizi makubwa ya umeme ambavyo ni Viyoyozi Majokofu, Runinga, Feni pamoja na Mota za umeme.

"Watu wengi wamekuwa wakitumia vifaa mbalimbali majumbani na maeneo mengine bila kufahamu kiwango halisi cha umeme kinachotumika katika vifaa, hivyo kuwepo kwa maabara hiyo nchini, kutasaidia kupima vifaa hivyo na kujua matumizi fanisi ya nishati na hivyo kuokoa gharama katika matumizi" Amesema Mha. Luoga

Mha. Luoga amesema kuwa maabara hizo zitakuwa na jukumu la kupima na kuthibitisha ubora na ufanisi wa vifaa vya umeme vinavyoingizwa nchini, kudhibiti bidhaa duni zisizo na viwango,kutoa ithibati kwa wazalishaji wa ndani na kusaidia Serikali katika usimamizi wa soko.

Mha. Luoga amefafanua kuwa maabara hizo zinathamani ya zaidi ya Euro milioni 1.8 (takriban shilingi bilioni 5).

Amesema kwa mara ya kwanza, Tanzania itakuwa na uwezo wa ndani wa kuhakikisha bidhaa zote zinakidhi viwango vya kitaifa na vya kikanda kabla ya kufika kwa mlaji.

Amesema uundaji wa viwango hivyo umehusisha Wataalam kutoka taasisi zaidi ya 10 zikiwemo Wizara ya Nishati, TBS, TANESCO, EWURA, REA, TIRDO, DIT, UDSM, ATC, NCC, TAREA na sekta binafsi.

Ameongeza kuwa kwa ushirikiano wa kitaalamu na Mshauri wa Kimataifa, viwango vya kiyoyozi na majokofu vimeidhinishwa rasmi kuwa viwango vya Kikanda vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), hatua inayowezesha Tanzania kuwa sehemu ya soko la kikanda lenye bidhaa zenye ubora na ufanisi wa nishati.

Uanzishaji wa MEPS na maabara hizi unalenga kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Taifa (2015), Mkakati wa Taifa wa Matumizi Bora ya Nishati (NEES 2024–2034) na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

Katika hatua nyingine , Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanza juhudi za kuandaa viwango katika teknolojia ya kupikia kwa kutumia nishati Safi ili kuendana na Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia (2024–2034).

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Upimaji na Huduma za Metrolojia wa TBS, Ridhiwani Matange ametoa wito kwa watanzania kutumia vifaa ambavyo vitakuwa vimepimwa katika maabara hizo.

Amesema elimu zaidi itatolewa kwa wananchi ili kuwajengea uwezo wa uelewa juu ya maabara hizo na viwango fanisi vinavyohitajika katika matumizi yao ya kila siku.

Naye Mkuu wa Ushirikiano wa Umoja wa Ulaya, Arc Stalmans na Msaidizi wa Mwakilishi Mkazi, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) Gertrude Lyatuu waamesisitiza kuwa wataendela kushirikina na Serikali ya Tanzania katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo hususan mradi huo wa matumizi bora ya nishati ili kupunguza hewa ya ukaa ili kulinda Mazingira.

# DKT. MATARAGIO AONGOZA WADAU UTOAJI MAONI MPANGO WA MATUMIZI YA GESI ASILIA NCHINI (NGUMP)

- Unalenga Kuchochea matumizi ya Gesi Asilia nchini
- Kuainisha matumizi ya Gesi Asilia kwa sekta mbalimbali katika kipindi cha miaka 25 kuanzia sasa
- Wadau waomba uharakishaji mikopo kwa wawekezaji Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia
- Kuangazia masoko ya Gesi Asilia ndani na nje ya nchi



Picha ya Pamoja viongozi mbalimbali katika Warsha iliyofanyika jijini Dar es Salaam iliyoandaliwa na Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) na kuhusisha wadau kutoka serikalini, sekta binafsi pamoja na Washirika wa Maendeleo.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio amefungua warsha ya wadau iliyolenga kuchambua na kutoa maoni kuhusu Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia nchini (NGUMP) kwa kipindi cha miaka 25 kuanzia sasa.

Mpango huo utaonyesha kiasi halisi cha matumizi ya gesi asilia kinachohitajika katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika sekta ya viwanda, uzalishaji wa umeme, sekta ya usafirishaji pamoja na matumizi ya nyumbani

Warsha hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam imeandaliwa na Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) na kuhusisha wadau kutoka serikalini, sekta binafsi pamoja na Washirika wa Maendeleo.

"Mradi huu wa NGUMP utatuwezesha kufahamu kiasi halisi cha matumizi ya gesi asilia katika maeneo mbalimbali hivyo itakuwa rahisi kufahamu

na kutenga kiasi cha gesi asilia inayohitajika katika eneo husika," amsema Dkt. Mataragio

Ameongeza kuwa NGUMP itasaidia kuona namna bora ya kuendeleza miundombinu ya gesi ya asilia nchini pamoja na kutafuta masoko ya gesi asilia ndani na nje ya nchi pia kuangalia mchango wa gesi hiyo katika uchumi wa nchi.

Vilevile amesema NGUMP itarahisisha utekelezaji wa DIRA ya Maendeleo ya 2050 kwa kuwa Gesi asilia ipo katika Sekta ya Nishati ambayo ni kichocheo cha pili Kati ya vitano vya kufanikisha matokeo ya Dira.

Aidha amesema NGUMP itatekeleza mpango mkakati wa Matumizi Nishati Safi ya Kupikia na Sera ya Nishati ya mwaka 2015.

Mhandisi John Bura ni mmoja ya washiriki katika warsha hiyo ambaye amesema kuwa mpango huo utasaidia kuchochea matumizi ya gesi asilia, pamoja na kuongeza kiwango cha matumizi ya gesi nchini.

Bura ameiomba Serikali pamoja na Taasisi za Fedha kuharakisha utoaji wa mikopo kwa wawekezaji hasa wa ndani wanaotaka kuwekeza katika maeneo mbalimbali kwenye sekta hiyo ili kusogeza huduma hiyo kwa wananchi kwa lengo la kupata matokeo mazuri yenye tija zaidi.

Hatua ya utoaji utoaji maoni ya NGUMP imefikwa baada Wizara ya Nishati na JICA kukamilisha rasimu ya NGUMP kupitia Mradi wa kujenga uwezo katika matumizi ya Gesi Asilia na kuongeza uzalishaji.

# ELIMU YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA YAWAFIKIA MAAFISA DAWATI NGAZI YA MIKOA NA HALMASHAURI

- Lengo ni kuwa na uelewa wa pamoja katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia.
- Mafunzo kuhusisha mikoa 26 na Halmashauri zake

Wizara ya Nishati imeanza kutoa elimu kuhusu Nishati Safi ya Kupikia kwa Maafisa Dawati wa Nishati Safi ya Kupikia ngazi ya mikoa na halmashauri kwa lengo la kuwa na uelewa wa pamoja katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia pamoja na kuwawezesha Maafisa Dawati kutambua majukumu yao katika utekelezaji wa mkakati.

Akifungua mafunzo hayo, wilayani Kibaha mkoani Pwani, Mwakilishi wa Katibu Tawala wa Mkoa wa Pwani, Bi. Hadija Mruma ameipongeza Wizara ya Nishati kwa jitihada mbalimbali inazochukua kwa vitendo katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini mojawapo ikiwa ni kuhakikisha elimu na vifaa vya nishati safi ya kupikia vinafika hadi ngazi za Mikoa, Halmashauri na Vijiji.

Ameeleza kuwa Mkoa wa Pwani unachukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa wanachi wanatumia nishati safi ya kupikia katika ngazi ya taasisi, kaya n.k


Bi. Hadija Mruma akipongeza Wizara ya Nishati kwa jitihada mbalimbali inazochukua kwa vitendo katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini mojawapo ikiwa ni kuhakikisha elimu na vifaa vya nishati safi ya kupikia vinafika hadi ngazi za Mikoa, Halmashauri na Vijiji.

akitoa mfano kuwa asilimia 76 ya taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 mkoani humo zimeshahamia kwenye nishati safi ya kupikia.

Aidha, amewapongeza Watendaji wa Wakala wa Nishati Vijijini ( REA) ambao wanashirikiana na




Maafisa wa Dawati wa Nishati Safi ya Kupikia ngazi ya mikoa na halmashauri wakipewa mafunzo lengo ni kuwa na uelewa wa pamoja katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia pamoja na kuwawezesha Maafisa Dawati kutambua majukumu yao katika utekelezaji wa mkakati..

Mkoa wa Pwani kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ikiwemo utoaji mitungi ya gesi kwa bei ya ruzuku.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia kutoka Wizara ya Nishati, Bw. Ngereja Mgejwa ameeleza kuwa mafunzo kuhusu Nishati Safi ya Kupikia yameanza kutolewa wilayani Kibaha, mkoani Pwani kwa kuhusisha Mikoa ya Pwani, Morogoro, Dar es Salaam, Mtwara, Lindi na Tanga.

Ameongeza kuwa, elimu ya nishati safi ya kupikia itaendelea kutolewa kwa Maafisa Dawati wa Nishati Safi ya Kupikia katika mikoa mingine iliyosalia kwani lengo ni kutoa elimu husika katika Mikoa yote 26 pamoja na Halmashauri zake.

Amesema kuwa suala la matumizi ya nishati safi ya kupikia ni kipaumbele cha nchi na dunia kwa ujumla ili kuondokana na athari zake katika mazingira, afya na kiuchumi.

Naye, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kutoka Wizara ya Nishati, Bi. Neema Mbuja ameeleza kuwa mafunzo yanayotolewa kwa maafisa dawati hao yanahusisha pia masuala ya Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano wa Nishati Safi ya Kupikia.

Ameeleza kuwa ili kufikisha elimu kwa wananchi kuhusu nishati safi ya kupikia ni muhimu maafisa dawati hao wakafahamu njia za mawasiliano zitakazowasadia kufikisha elimu na jumbe zitakazotumika kuendana na maeneo wanayoyasimamia.

Ameongeza kuwa uwepo wa Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano wa Nishati Safi ya Kupikia (National Clean Cooking Communication Strategy) unatoa mwongozo wa namna wadau watakavyoshirikiana kutoa elimu kwa umma ili kuondoa dhana potoshajii (misconception) kuhusu nishati safi ya kupikia na kubadili mitazamo hasi kuwa chanya kwa lengo la kuleta mabadiliko katika utekelezaji wa ajenda ya kitaifa ya nishati safi ya kupikia.

# WIZARA YA NISHATI YAKAGUA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA KWA TAASISI ZINAZOLISHA WATU ZAIDI YA 100 ILEMELA.

- Lengo ni kuhakikisha Taasisi za Umma na Binafsi zinatekeleza agizo la Serikali la kutumia Nishati Safi ya Kupikia
- Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia ahimiza Wakurugenzi wa Halmashauri/Manispaa kuhakikisha agizo hilo la Serikali linatekelezwa
- Awaasa Walimu kufundisha Wanafunzi juu ya Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia



Mkurugenzi wa Nishati safi ya Kupikia, Nolasco Mlay alipofanya ziara mkoani Mwanza kwa kukagua shule tatu za Sekondari katika Manispaa ya Ilemela

Mkurugenzi wa Nishati safi ya Kupikia, Nolasco Mlay pamoja na Wataalam kutoka Wizara ya Nishati wameanza ziara ya kikazi mkoani Mwanza kwa lengo la kukagua utekelezaji wa agizo la Serikali kwa Taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 kutumia Nishati Safi ya Kupikia.

Ziara hiyo imeanza kwa kukagua shule tatu za Sekondari katika Manispaa ya Ilemela ambazo zimeanza kutumia Nishati Safi ya Kupikia baada ya kunufaika na mradi wa CookFund kupitia mpango wa kimataifa wa Integrated Approach to Sustainable Clean Cooking Solution unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Mitaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF) kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU).

Ziara hiyo pia inalenga kufanya tathmini ya matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwa taasisi zinazopokea ufadhili kutoka mradi wa CookFund.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Bw. Nolasco Mlay amesema kuwa ziara hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024–2034), ambao unalenga kuhakikisha taasisi za umma ikiwemo shule, zinatumia teknolojia salama na rafiki kwa mazingira katika upishi.

Katika kuhakikisha kuwa agizo hilo la Serikali linatekelezwa kwa mafanikio, Mlay amewasisitiza Wakurugenzi wa Halmashauri na Manispaa ambao bado taasisi katika maeneo yao hazijahama kutoka matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia kuhakikisha kuwa wanatekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.




Picha ya Pamoja ya ziara iliyofanyika Jijini Mwanza kutembelea shule zilizonufaika na mradi wa CookFund kupitia mpango wa kimataifa wa Integrated Approach to Sustainable Clean Cooking Solution unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Mitaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF) kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU).

"Taasisi za Umma na Binafsi katika maeneo yenu kama vile Shule, Hospitali, Magereza pamoja Jeshi zinapaswa kutumia teknolojia salama na rafiki kwa mazingira katika upishi ili kuepusha athari za kiafya na kimazingira kwa nchi." Amesema Mlay

Sambamba na hilo, Mlay amewahimiza Walimu na Wakuu wa Shule kuwa mstari wa mbele kuwaelimisha wanafunzi juu ya faida ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ili wawe mabalozi wa kuelimisha wengine.

Akizungumza kwa niaba ya Afisa Elimu Sekondari Manispaa ya Ilemela, Afisa Elimu Maalum wa Manispaa hiyo amepongeza utekelezaji wa mkakati wa matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia unaoendelea katika Manispaa ya Ilemela akiahidi kuwa Manispaa hiyo itaendelea kutekeleza agizo hilo ambapo kwa sasa tayari kuna shule kumi ambazo zipo kwenye mpango huo wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Vilevile, Walimu Wakuu wa Shule zilizokaguliwa wameeleza kuwa matumizi ya nishati safi ya kupikia yamesaidia shughuli za upishi kufanyika katika mazingira rafiki na salama, kuokoa muda na kuwa na gharama nafuu.

Katika hatua nyingine, Wataalam kutoka Wizara ya Nishati walitembelea shule ambazo bado hazijaanza kutumia nishati safi ya kupikia na kuwaasa Viongozi wa shule hizo zinazotegemea kuni na mkaa kuanza kuboresha mifumo yao ya upishi na kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Shule tatu zilizotembelewa katika Manispaa ya Ilemela ambazo zinatumia Nishati Safi ya Kupikia ni pamoja na Shule ya ufundi ya Wavulana ya Bwiru Sekondari, Shule ya Wasichana ya Bwiru Sekondari pamoja na Shule ya Sekondari ya Buswelu.

# WIZARA YA NISHATI YAFANYA UKAGUZI WA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA SHULE ZA KARATU

- Lengo ni kuhakikisha agizo la Serikali kwa taasisi kutumia Nishati Safi ya Kupikia linatekelezwa
- Asisitiza Wakurugenzi wa Halmashauri kushirikiana na Wakuu wa Shule/Wadau kufanikisha agizo la matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia



Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia, Bw. Nolasco Mlay akizungumza na Mwalimu mara baada ya kutembelea Shule Wilayani Karatu mkoani Arusha

Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia, Wizara ya Nishati, Bw. Nolasco Mlay ametembelea jumla ya shule sita wilayani Karatu mkoani Arusha lengo likiwa ni kukagua utekelezaji wa agizo la Serikali kwa Taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 kutumia Nishati Safi ya Kupikia.

Mlay amesema kuwa ziara hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024–2034), ambao unalenga kuhakikisha taasisi za umma ikiwemo shule, zinatumia teknolojia salama na rafiki kwa mazingira katika upishi.

Akizungumza na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Karatu, Juma Hokololo, Mlay amesisitiza kuhusu Wakurugenzi wa Halmashauri







Zoezi la uandaaji wa Chakula cha wanafunzi likiendelea katika moja ya shule zilizotembelewa na Mkurugenzi wa Nishati Safi ya kupikia Bw. Nolasco Mlay.

kushirikiana na Wakuu wa Shule, Wazazi na Wadau mbalimbali ili kuweza kujenga majiko ya kisasa ambayo yanatumia nishati zilizo salama.

Kwa shule ambazo zipo katika hatua za awali za ujenzi wa miundombinu ya nishati safi ya kupikia amezisisitiza kuhusu kuhakikisha kuwa agizo la Serikali linatekelezwa kwa wakati ili kulinda afya za wapishi lakini pia kupunguza gharama za manunuzi ya nishati zisizo salama na kulinda mazingira.

Sambamba na hilo, Mlay amewahimiza Walimu kuwa mstari wa mbele kuwaelimisha wanafunzi juu ya faida za matumizi ya nishati safi ya kupikia ili wawe mabalozi wazuri wa kuelimisha wengine.

Tunawaomba walimu kuelekeza wanafunzi kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia kama vile gesi, majiko banifu na umeme kama njia mbadala za kuni na mkaa kwani watoto hawa wanapojifunza watasaidia kubadilisha mitazamo ya jamii kutoka kwenye matumizi ya nishati isiyo safi na kutumia nishati safi ya kupikia". Amesisitiza Mlay

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Karatu, amemshukuru Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia kwa ziara hiyo na kuahidi kuwa atasimamia utekelezaji wa agizo la Serikali la matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Baadhi ya shule za zilizotembelewa na Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia wilayani Karatu ni Ganako Sekondari, Gyekrum Arusha, Karatu Sekondari, Ayalabe Sekondari, Welwel Sekondari pamoja na shule ya msingi Ganako.

# KATIBU MKUU NISHATI ARIDHISHWA NA KASI YA UTEKELEZAJI MRADI WA UMEME JUA KISHAPU

- **Utekelezaji wafikia asilimia 80.4**
- **Awamu ya kwanza kukamilika Desemba 2025**
- **Mhandisi Mramba asema ni jitihada za Rais Samia kuhakikisha wananchi wanapata nishati safi, salama na nafuu**



Wataalamu mbalimbali walipo tembelea Ujenzi wa mradi wa usafirishaji umeme wa msongo wa kilovoti 400 unaounganisha Tanzania na Zambia (TAZA) umefikia asilimia 58 ya uekelezaji wake kwa upande wa Tanzania.

Serikali kupitia Wizara ya Nishati imeeleza kuridhishwa kwake na kasi ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa kitaifa wa kuzalisha umeme jua (150MW) katika Wilaya ya Kishapu, mkoani Shinyanga ambao hadi sasa umefikia asilimia 80.4 ya ujenzi.

Baada ya kukagua maendeleo ya mradi huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, amesema Serikali inaridhishwa na hatua zilizofikiwa na mkandarasi, akibainisha kuwa mradi huo ni sehemu ya utekelezaji wa malengo ya kitaifa na kimataifa ya upatikanaji wa nishati endelevu.

Mhandisi Mramba ameeleza kuwa mradi huo wa megawati 150 unatekelezwa kwa awamu mbili kwa gharama ya Shilingi bilioni 323.

Amesema kuwa awamu ya kwanza ya mradi huo itakamilika desemba 2025 kwa kuanza kuzalisha megawati 50 huku Kampuni ya Sinohydro kutoka China ikiwa ndiyo mkandarasi mkuu wa mradi



" Mradi huu ni sehemu ya jitihada za Serikali chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye anaendelea kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanapata huduma ya nishati safi, salama na nafuu." Amesisitiza Mhandisi Mramba

Ameongeza kuwa, kukamilika kwa mradi wa umeme jua wa Kishapu kutazidi kutengemaza upatikanaji wa umeme mijini na vijijini na kupunguza utegemezi wa vyanzo vya nishati visivyo rafiki kwa mazingira.

Kwa upande wake, Mhandisi Msimamizi wa Mradi, Emmanuel Anderson amesema kasi ya ujenzi ni nzuri na wanatarajia



Picha ya Pamoja baada ya kukagua maendeleo ya mradi huo mkubwa wa kitaifa wa kuzalisha umeme jua (150MW) katika Wilaya ya Kishapu, mkoani Shinyanga ambao hadi sasa umefikia asilimia 80.4 ya ujenzi.

# WANAFUNZI WA KIKE 10 WAPATA UFADHILI WA MASOMO KATIKA MASUALA YA NISHATI ENDELEVU

- **Ni kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Ubalozi wa Ireland**
- **Ufadhili huo ni utekelezaji wa Mpango Kazi wa mwaka 2018 wa Matumizi Bora ya Nishati**
- **Mkurugenzi wa Utawala Wizara ya Nishati ashukuru UNDP na Ubalozi wa Ireland kwa ufadhili**

Wanafunzi 10 wa kike nchini wamepata ufadhili wa masomo katika masuala ya Nishati Endelevu kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Ubalozi wa Ireland katika mwaka wa fedha 2025/2026 ikiwa ni matokeo ya ushirikiano uliopo kati ya Wizara ya Nishati na UNDP katika kuwajengea uwezo Wanawake wa Tanzania katika masuala ya Nishati.

Kutolewa kwa ufadhili huo ni utekelezaji wa Mpango Kazi wa mwaka 2018 wa Matumizi Bora ya Nishati ambapo pamoja na masuala mengine, suala la kuwajengea uwezo wanawake katika masuala ya nishati limeainishwa.

Akizungumza katika hafla ya kuwapongeza Wanafunzi hao jijini Dar es saalam, Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati ambaye ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Bi. Ziana Mlawa amesema kuwa kutolewa kwa ufadhili huo kunawawezesha Wanawake wa Tanzania kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa mfumo wa nishati endelevu na rafiki kwa mazingira huku kukiwa na kiwango kidogo cha uzalishaji wa hewa ukaa.

Mlawa ameeleza kuwa, Serikali, kupitia Wizara ya Nishati, imeendelea kuwawezesha wanawake katika masomo ya nishati, hususan katika ngazi ya elimu ya juu.

Vilevile, kupitia ushirikiano na wadau wake mbalimbali wakiwemo Ubalozi wa Ireland na Shirika la Maendeleo la Umoja



Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati ambaye ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Bi. Ziana Mlawa akihutubia umati wa watu.

wa Mataifa (UNDP), imeendelea kuweka kipaumbele katika uwekezaji wa upatikanaji wa elimu ya juu na masuala ya uongozi kwa wanawake.

Ameongeza kuwa, tangu kuanza kutolewa kwa ufadhili wa masomo katika sekta ya Nishati kupitia Mpango Kazi wa mwaka 2018 wa Matumizi Bora ya Nishati wanafunzi wa kike takriban 35 wamenufaika na ufadhili wa masomo katika mwaka 2023/2024 na 2024/2025.

Mlawa ameishukuru UNDP na Ubalozi wa Ireland kwa kutoa ufadhili huo wa masomo ambao mwaka huu unafikia ukomo wake huku akiwaomba kuendelea kutoa ufadhili wa masomo hayo ambayo ni muhimu katika ukuaji wa Sekta ya Nishati.

Pia amekishukuru Chuo cha DIT ambacho ndicho kitatoa mafunzo kwa wanafunzi waliofadhiliwa.

Mlawa pia amewapongeza Wanafunzi wa kike waliopata ufadhili akiahidi kuwa Wizara iko tayari kushirikiana nao, kuwasaidia na kuwapatia majukwaa ambapo mawazo yao na ubunifu wao utasikika na kuthaminiwa.



# KATIBU MKUU NISHATI AHIMIZA UZALENDO NA UADILIFU KWA WANACHAMA WA EWURA CCC

- Azindua Baraza la Tatu la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba, akitoa wito kwa wajumbe wa Baraza jipya la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA Consumer Consultative Council – EWURA CCC)

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba, ametoa wito kwa wajumbe wa Baraza jipya la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA Consumer Consultative Council – EWURA CCC) kuwa na nidhamu, uzalendo na uwajibikaji katika majukumu yao, ili kuongeza ufanisi wa kazi na kuleta manufaa kwa wananchi.

Akizungumza jijini Mwanza wakati wa uzinduzi wa Baraza jipya la tatu la EWURA CCC pamoja na mafunzo kwa wajumbe wapya, Mha. Mramba amewahimiza wajumbe hao kufanya kazi kwa ushirikiano na kuweka mbele maslahi ya taifa.

“Ni muhimu kila mjumbe kuwa mfano wa uwajibikaji na uadilifu. Baraza hili lina jukumu kubwa la kusikiliza na kuwasemea watumiaji wa huduma za nishati na maji, hivyo nidhamu na uzalendo ni nguzo kuu za mafanikio.” Amesema Mhandisi Mramba

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa EWURA CCC, Bi. Stella Lupimo, alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo wajumbe wapya ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, hususan katika kusimamia masuala yanayohusu haki na usalama wa watumiaji wa huduma hizo.

Naye Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mha. Poline Msuya, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya wadau wote wa sekta ya nishati ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora, nafuu na endelevu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Bw. Hassan Minga, aliahidi kuwa baraza hilo jipya litajikita zaidi

katika kusikiliza changamoto za wananchi na kuzifikisha kwa mamlaka husika kwa ajili ya utatuzi.

Uzinduzi wa baraza jipya la tatu la EWURA CCC na mafunzo hayo ni sehemu ya mkakati wa serikali wa kuimarisha uwajibikaji, uwazi na uadilifu katika usimamizi wa sekta za nishati na maji, ili kuleta tija na maendeleo kwa jamii.




# DKT. MATARAGIO AAGIZA VIFAA VYOTE VYA UHAKIKI WA JOTOARDHI ZIWA NGOZI KUFIKA KWA WAKATI

- **Ni baada ya kukagua mradi na kukuta baadhi ya vifaa bado havijafika**
- **Asisitiza mradi kukamilika kwa wakati ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Nishati ya mwaka 2015**
- **Kazi ya uhakiki wa Jotoardhi Ziwa Ngozi yafikia asilimia 60**


Picha ya Pamoja ya viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati wakiwa na wataalamu wengine mara baada ya kutembelea na kukagua kazi zinazoendelea kutekelezwa na mradi huo wilayani Rungwe mkoani Mbeya.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Kampuni yake Tanzu ya Uendelezaji Jotoardhi (TGDC) kuhakikisha kuwa vifaa vyote vya uhakiki wa rasilimali Jotoardhi katika mradi wa Ziwa Ngozi vinafika kwa wakati ili kazi za uhakiki ziweze kumalizika kulingana na muda uliopangwa.

Dkt. Mataragio ametoa maagizo hayo wakati wa ziara yake ya kukagua kazi zinazoendelea kutekelezwa katika mradi huo wilayani Rungwe mkoani Mbeya.


Madhari nzuri na yakuvutia namna Ziwa Ngosi linavyoonekana lililopo Wilayani Rungwe Mkoani Mbeya.

“Huu mradi mnapaswa kuukamilisha kwa wakati kutokana na umuhimu wake nchini, tunapotekeleza miradi hii ya Jotoardhi tukumbuke kuwa tunatekeleza pia Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015 ambayo inasema Tanzania inapaswa izalishe umeme kwa kutumia vyanzo mchanganyiko (generation mix) ambapo jotoardhi ni mojawapo.” Amesema Dkt. Mataragio

Kuhusu suala la vifaa vya uhakiki kuchelewa kufika katika eneo la mradi la Ziwa Ngozi ambalo litazalisha umeme wa megawati 70, Dkt. Mataragio ameagiza kuwa vifaa vyote vya mradi vinunuliwe na kufika eneo la mradi kwa mara moja.

Dkt. Mataragio ameeleza kuwa, utekelezaji wa miradi ya Jotoardhi imeainishwa pia katika Mpango wa Taifa wa Nishati (National Energy Compact) ambao unaishia 2030 ambapo Tanzania inatakiwa kuwa na megawati 130 zinazotokana na rasilimali ya jotoardhi, pia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050 inaelekeza nchi kuwa na vyanzo mchanganyiko vya kuzalisha umeme.

Kwa upande wake, Meneja Mkuu wa TGDC, Mha. Mathew Mwangomba ameeleza kuwa maagizo yaliyotolewa na Serikali yatatekelezwa kwa ufanisi ili kukamilisha mradi kwa wakati.

Akielezea maendeleo ya uhakiki wa rasilimali jotoardhi katika mradi huo, Mha. Mwangomba amesema umefikia asilimia 60 ili kuweza kufikia hifadhi ya jotoardhi.

“Tunategemea ndani ya miezi sita tutakamilisha uhakiki katika visima vyote vitatu”. Amesema Mha. Mwangomba

Katika ziara hiyo Naibu Katibu Mkuu aliambatana na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Mha. Innocent Luoga na watendaji wa Wizara ya Nishati na TANESCO.

# MATUKIO KATIKA PICHA

## SIKU YA CHAKULA DUNIANI






Picha mbalimbali za matukio katika wiki ya maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani kitaifa yaliyofanyika Mkoani Tanga kuanzia tarehe 10 Oktoba hadi 16 Oktoba 2025 na kuhudhuriwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa mara baada ya kutembelea Banda la Wizara ya Nishati na Tasisi zake amepongeza utekelezaji na usimamizi miradi mbalimbali ya nishati nchini.







Katika maadhimisho hayo ya Siku ya Chakula Duniani yaliyoanza tarehe 10 Oktoba 2025 yamepelekea wananchi kupata elimu kuhusu mafanikio ya sekta ya nishati na miradi inayoendelea huku wananchi 500 wakinufaika na mitungi ya gesi iliyokuwa ikiuzwa kwa bei ya Ruzuku ya shilingi 17,500/= Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu amekabidhi tuzo kwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ikiwa ni kupongeza juhudi za taasisi hiyo kupitia maadhimisho hayo ya Siku ya Chakula Duniani.







For more info
**www.nishati.go.tz**

